zana zaidi za kumshindia Ibilisi na mashetani wake.

Mazingira haya yakawasaidia kupata msaada makhsus wa kimbingu pale waliporuhusiwa kukabiliana kivita na maadui zao kiasi ya kwamba wakaahidiwa kuweza kuwashinda makafiri hata mia mbili juu ya wao wenyewe kuwa ishirini tu. Na hali hiyo waliishuhudia katika vita vya Badri ambapo Waislamu 313 walikabiliana na maadui 1000 waliosheheni zana kali za kivita wakiwa na majenerali shujaa waliovaa deraya za chuma na hata hivyo wakaweza kuwashinda. Mungu Alishaahidi kuwa Anao uwezo wa kuwasaidia wale wafanyao Jihadi ya kweli.

Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya imekuja kuturejesha kwenye mafundisho halisi ya Kiislamu kama yalivyofundishwa na Mtume Muhammad s.a.w. Hatua ya kwanza aliyochukua mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ilikuwa ni kuwafundisha wafuasi wake Qurani Tukufu kwa maelezo makhsus yaliyoambatana na msaada makhsus wa funuo za Mwenyezi Mungu. Mafundisho hayo yaliwanyanyua wafuasi wake katika madaraja ya juu kabisa ya ucha Mungu na kuweza kudhihirisha subira za kiwango cha juu zilizowakurubisha zaidi kwa Mwenyezi Mungu. Lengo la jihadi sawa na mafundisho ya Qurani Tukufu ni pamoja na kulinda nyumba za ibada za watu wa dini mbali mbali yakiwemo makanisa, mahekalu na misikiti. Qurani imekataza kulazimishana katika mambo ya dini na kila mtu anao uhuru wa kuingia na kutoka dini yoyote ikiwemo Islamu. Islamu haina adhabu ya kifo kwa yule anayeiritadi au kuachana nayo. Wanazuoni wa Kiislamu wameipotosha maana halisi ya Jihadi kwa kufanya kwayo yale yaliyokatazwa na Islam.

Njooni tujiunge na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya tufanye ile jihadi ya kupambana na Ibilisi na wafuasi wake tukiwa chini ya msaada makhsus wa Mwenyezi Mungu kwa kuambatana na Ukhalifa halisi ulioagizwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake s.a.w.

TOVUTI YETU: www.alislam.org.

**Taarifa za kituo chetu cha**

**MUSLIM TELEVISION AHMADIYYA (MTA)**

ambacho kinafanya kazi muda wote ni:-

**MTA FREQUENCY-12015.V**
**SYMBOL RATE - 29,950**
**SAT SES.5**

**Anuani :-**
Ukiwa na maswali zaidi unaweza kuwasiliana na wabashiri wetu wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya nchini kote, kwa:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Arusha/Kilimanjaro | 0787 770 655 |
| 2. | Dar es Salaam | 0655 105 096 |
| 3. | Dar es Salaam | 0620 124 768 |
| 4. | Dodoma/Singida | 0782 919 298 |
| 5. | Iringa | 0715 884 800 |
| 6. | Kagera | 0716 682 063 |
| 7. | Kigoma | 0716 045 918 |
| 8. | Mara | 0785 676 614 |
| 9. | Mbeya | 0714 266 800 |
| 10. | Morogoro | 0714 601 191 |
| 11. | Mtwara / Lindi | 0656 116 652 |
| 12. | Mwanza | 0788 677 509 |
| 13. | Pwani | 0623 228 033 |
| 14. | Shinyanga | 0788 676 618 |
| 15. | Songea | 0656 116 698 |
| 16. | Tabora | 0788 677 433 |
| 17. | Tanga | 0714 583 380 |
| 18. | Tunduru | 0655 028 203 |
| 19. | Zanzibar | 0675 321 543 |

لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ

**Hapana Apasaye kuabudiwa ila Allah**
**Muhammad ni Mtume wa Allah**

# JIEPUSHENI NA MAANA POTOFU ZA JIHADI

**Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania**
**P.O. Box 376, Dar es Salaam.**
**Mnazimmoja, barabara ya Bibi Titi.**
**Mkabala na Bustani ndogo ya Mnazimmoja**
**Email: ahmusjamtaz@gmail.com**

**Imechapishwa na:**
**Ahmadiyya Printing Press Tanzania**
**Mob: 0715 771 813**
**Email: ahmadiyyaprintingpresstz@gmail.com**

بســـــم الله الـرَّحـمــن الـرَّحــيــــــم

***Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu***

# JIEPUSHENI NA MAANA POTOFU ZA JIHADI

Dunia leo inashuhudia mauaji ya kikatili sana yanayotendeka kwa jina la dini. Mauaji ambayo dini zote imeyapinga. Jina takatifu la Jihadi linanajisiwa na baadhi ya Waislamu wachache kwa umwagaji damu wa kutisha sana. Anayejiita Khalifa wa Waislamu, aliyeanzisha kikundi cha wanamgambo kinachojiita ISIS na kuteka maeneo kadhaa ya Syria na Iraq, anawaita Waislamu wote duniani waende kula kiapo cha utii kwake na kufuata Uislamu wake uliovuka mipaka katika maasi na ukatili. Uislamu wa kuwaoa wanawake kwa nguvu na anayediriki kukataa ndoa hiyo ya kiubakaji kuuawa, kiasi ya kwamba mamia ya akina mama wameuawa kwa njia hiyo. Uislamu huo wenye nembo ya kiharamia kwa kuwateka watu nyara na kulazimisha fidia ya mamilioni ya fedha. Anataka watu wamfuate katika uislamu wake wa kuchinja watu hadharani, kuwachoma moto hadharani wakiwa wangali hai na kuwapiga picha za video na kuzisambaza duniani kote kwa njia ya mitandao. Uislamu wake umewafanya watu duniani kote waiogope na hata kuichukia Islam na kuwasababishia usumbufu mkubwa waislamu wa sehemu mbali mbali duniani.

Mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. anasema: “Maradhi ya kiroho, yaani utovu wa maadili mema, mawazo machafu, ukatili na utovu wa huruma vinaendelea miongoni mwa firqa (madhehebu) za Kiislamu ................ Huruma ya binadamu, majuto, kupenda haki, upole na unyenyekevu-sifa zote nzuri zinatoweka siku hadi siku, kana kwamba karibuni zitaiaga jamii. Ukatili huu na utovu huu wa maadili mema unawafanya Waislamu wengi waonekane kama wanyama wa porini. .................. wako wengi miongoni mwetu Waislam wanaomuua mtu asiye na hatia au kufanya mauaji yasiyokuwa na mipaka. Hawamuogopi Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu Ambaye Ameyakadiria maisha ya mwanadamu kuwa ya daraja la juu kuliko ya wanyama wote. Lakini huu ukatili na dhulma na utovu wa huruma vinasababishwa na nini? Vinasababishwa na jambo hili kwamba tangu wakati wa utoto wao, hekaya na hadithi na fikra zisizo sahihi za itikadi ya jihadi zinaimbwa ndani ya masikio yao na kushinikizwa ndani ya mioyo yao na matokeo yake pole pole wanakufa kiroho na hatimae kutohisi ubaya wa vitendo vyao vya kuchukiza, bali yule amuuaye mtu mwingine na kusababisha maangamizi kwenye familia ya mtu aliyeuawa hujidhani kwamba amefanya kitendo kinachostahili au tuseme hivi kwamba hujidhani ameitumia vema fursa ya kujipatia upendeleo kutoka katika jamii yake.

“Kwa kuwa hakuna mafundisho au hotuba zinazotolewa nchini mwetu kuuzuia uovu wa aina hiyo, na kama yapo mafundisho yoyote ya aina hiyo huwa ni yenye viini vya unafiki ndani yake, basi watu wa kawaida huwa na fikra za kuviunga mkono vitendo hivyo viovu. Hivyo basi, kwa kuwahurumia watu wangu, nimetunga vitabu kadhaa kwa lugha ya Kiurdu, Kiajemi na Kiarabu ambamo nimesema kwamba maoni yanayoshikiliwa na watu wote kuhusiana na jihadi, ambayo yamezagaa miongoni mwa Waislamu, yaani kusubiriwa kwa Imamu mwenye kumwaga damu aliyejawa na chuki na uadui kwa watu wengine, ni mfumo wa imani potofu zilizofundishwa na Masheikh wasioona mbali; vinginevyo Islam hairuhusu utumiaji wa upanga kuieneza imani hii; isipokuwa wakati wa vita vya kujihami au wakati wa vita zinazopiganwa ili kumwadhibu mdhalimu au kutetea uhuru. Haja ya kuwepo kwa vita ya kujihami inakuja wakati ambapo uchokozi wa adui unahatarisha maisha ya mtu. Basi hizo ndizo aina tatu za jihadi zinazoruhusiwa na sheria, na kinyume cha hizi aina tatu, hakuna aina nyingine ya vita inayoruhusiwa na Islam katika kuieneza imani.....” (Yesu katika India uk 7-8).

Jihadi yenyewe ya Islamu inaagiza kinyume kabisa na hayo wayatendao hao wanaojiita waislamu kama vile Boko Haram, Al Shabab n.k. Mtume Muhammad s.a.w. alisema kwamba Jihadi kubwa kabisa kuliko zote ni ile Jihadi ya kupambana na Ibilisi kwa kumnyang’anya udhibiti wa nafsi yako anayoielekeza kwenye maovu. Jihadi ambayo aliita kwa jina la *Jihaadul Akbar*. Njia ya kuipata kikamilifu Jihadi hii ni kwa kupitia Jihadi nyingine iitwayo *Jihadun Kabiir,* ambayo ni Jihadi ya kuyatumia na kuyatekeleza kikamilifu maagizo ya Qurani Tukufu yenye kukataza kabisa maasi ya kila aina yakiwemo ukatili, mauaji, ubakaji, utekaji nyara n.k.

Mtume Muhammad s.a.w. aliidhihirisha Jihadi hii kwa miaka 13 mfululizo katika maisha yake ya awali ya utume wakati akiwa Makka, kwa kuonyesha uvumilivu wa hali ya juu kabisa. Yeye na wafuasi wake walipata kila aina ya mateso na udhia, na wengine wao kuuawa kikatili kabisa, lakini wakaonyesha subira ya hali ya juu kabisa. Ingawa alitendewa unyama wote huo, lakini alionyesha upendo wa hali ya juu sana kwa hata maadui zake, hali iliyowafanya wengi zaidi kujiunga na dini ya Kiislamu kwa kuona upendo huo usio na kifani. Walidhihirisha ucha Mungu wa hali ya juu kabisa uliowavuta Malaika toka mbinguni kuja kuwasaidia, kuwapa moyo na kuwahami. Waliweza kabisa kumshinda Ibilisi aliyewanyemelea katika kila kona na hivyo kuzawadiwa uteremsho wa Malaika wa Mwenyezi Mungu walioteremka na